JINSI KIJANA ALIYEOKOKA ANAVYOWEZA KUJENGA NGOME ZA UTAJIRI UDUMUO KABLA YA KUFIKIA UMRI WA MIAKA 35
Mwl. Obed J.V. Milinga (CFE)
(Dodoma, Tanzania.)
June 2026
AKIBA
UWEKEZAJI
ELIMU
STRONG FINANCIAL HOLDINGS

=======================================

SEMINA YA JINSI KIJANA ANAVYOWEZA KUJENGA NGOME IMARA ZA UCHUMI NA MAFANIKIO KIFEDHA KABLA YA UMRI WA MIAKA 35.

Na Mwl. Obed Venerando Milinga (Dodoma, Tanzania.)

Email: milinga2015@gmail.com

Simu ya Whatsapp: **0768201749**

Simu kawaida: **0767285417**

Mada iliyotolewa kwenye Semina ya Vijana wa Makanisa Jijini Mwanza

Tarehe 18-19 Juni 2016.

DAY ONE:

SOMO LA 1: KWA NINI VIJANA WALIOOKOKA WENGI NI MASKINI KIFEDHA

Utangulizi:

Moja ya changamoto kubwa kwa vijana wa kipentekoste ni kutofanya mapinduzi ya kiuchumi na kifedha katika umri wao wa ujana.

Changamoto hii siyo kwa vijana peke yake. Bali ni kanisa zima la Tanzania kama siyo Afrika yote. Masomo ya fedha na uchumi yameonekana kuwa siyo sehemu ya masomo muhimu katika silabasi za masomo ya makanisani. Wapo viongozi wengi wasiopenda mafundisho haya makanisani mwao mpaka leo.

Lakini kama tunataka kuleta mapinduzi ya kiroho, Vijana wa Kipentekoste hatuna budi kuleta mapinduzi ya kifedha na kiuchumi katika makanisa ya Tanzania kwanza ndipo Afrika itawezekana kubadilishwa. Hatuwezi kubadilisha Tanzania kiroho mpaka tubadilike kifedha.

Itakuwa vigumu sana kuleta mapinduzi ya kiroho makanisani kama suala la maarifa ya kifedha tutakuwa hatuyafundishi madhabahuni na kukataa maarifa ya kifedha kwa visingizio kwamba waumini wanaacha kusali wakipata fedha. Bila maarifa ya fedha ndani yetu ulimwengu utatukataa. Mungu naye atatukataa pia (Hosea 4:6).

Katika semina hii ya masa 4 ambapo leo nitatumia masaa 2 na siku ya pili masaa 2 pia, tutaangazia mambo makuu yafuatayo: Mifano ya Vijana wa Biblia waliofanya mapinduzi ya kiuchumi na kifedha nyakati zao na mpaka leo vizazi vyote vinajifunza kwao, Sababu 10 ambazo zinasababisha vijana wa Kipentekoste kuwa maskini, Mbinu 4 walizotumia Vijana wa Zamani Kufanikiwa Kifedha na Kiuchumi, . Tutaangazia maarifa ya fedha, uwekezaji, biashara za kisasa na tabia mbalimbali zinazotukwamisha kuleta mapinduzi yetu wenyewe na kushindwa kuleta mapinduzi ya kiroho na kiuchumi kwa makanisa yetu.

Tutaona sababu zinazowakwamisha vijana wa kipentekoste mpaka kushindwa kujitoa kwenye umaskini wa kifedha na kiuchumi na kujikuta hawana matumaini ya maisha na hawana msaada kwa kanisa, kwa familia zao na kwa taifa.

A. Mfano wa Vijana 10 wa Biblia waliofanikiwa Sana Kifedha na Kiuchumi.

Ifuatayo ni orodha ya vijana 10 waliofanikiwa kiuchumi na kifedha enzi za Biblia ambao tunaweza kujifunza kwao ili nasisi tufanikiwe. Orodha hiyo ni kama ifuatavyo:

1. Kijana Sulemani
Akiwa kijana mdogo sana aliporithi kiti cha enzi kutoka kwa baba yake, Mungu alimpa hekima. Alikuwa mtu tajiri zaidi aliyewahi kuishi, akikusanya dhahabu nyingi na kujenga miradi mikubwa.

"Hivyo mfalme Sulemani akawapita wafalme wote wa dunia kwa utajiri na hekima." (**1 Wafalme 10:23**).

2. Kijana Daudi
Alianza kama mchungaji mdogo wa kondoo wa familia yake. Mungu alimweka wakfu akiwa kijana, akapanda ngazi na kuwa mfalme aliyefanikiwa kijeshi na kiuchumi.

Maandiko yanasema: *"Bwana akawa pamoja naye kila aendako; naye Daudi akafanikiwa sana."* (**1 Samweli 18:14**).

3. Kijana Yusufu
Akiwa kijana wa miaka 17, alitupwa utumwani na gerezani. Hata hivyo, alifanikiwa sana katika mambo yote aliyoyafanya na hatimaye kuwa Waziri Mkuu wa Misri na msimamizi wa uchumi wa taifa hilo.

Biblia inasema hivi: *"Yusufu akafanikiwa, akawa mtu wa nyumbani mwake, yule bwana Mmisri... Naye bwana wake akaona ya kuwa Bwana yu pamoja naye, na ya kuwa Bwana anafanikisha mambo yote yaliyopita mkononi mwake."* (**Mwanzo 39:2, 3**).

4. Binti Esta (Hadassa)
Huyu dada alikuwa yatima na kijana mdogo wa Kiyahudi, alipata kibali na kuheshimika sana. Alifanikiwa kuwa Malkia wa Uajemi, nafasi iliyompa ushawishi mkubwa wa kiuchumi na mamlaka**:** *"Basi malkia Esta akapata kibali machoni pa watu wote waliomwona."* (**Esta 2:15**).

5. Kijana Danieli
Huyu kijana alichukuliwa mateka akiwa kijana mdogo. Kupitia maarifa, nidhamu na hekima ya Mungu aliyopewa, alifanikiwa na kupandishwa vyeo vya juu kiuchumi na kisiasa.

Tazama Biblia inavyosema: *"Basi mfalme akamwadhimisha Danieli, akampa zawadi nyingi na kuu, akamfanya awe mkuu juu ya mikoa yote ya Babeli, na msimamizi mkuu wa wote wenye hekima wa Babeli."* (**Danieli 2:48**).

6. Vijana Shadraka, Meshaki, na Abednego
Hawa walikuwa vijana wenzake Danieli walioshiriki naye utumwani. Walisimama imara katika imani yao, na hatimaye wakafanikiwa na kufanywa watawala wa mambo ya uchumi na utawala katika jimbo la Babeli.

Biblia inasema: *"Ndipo mfalme akawakuza Shadraka, na Meshaki, na Abednego, katika mkoa wa Babeli."* (**Danieli 3:30**).

7. Kijana Yosia
Alikua mfalme wa Yuda akiwa na umri wa miaka nane tu. Katika ujana wake, alifanya matengenezo ya kiroho na kiuchumi na kurejesha heshima ya nchi yake.

Biblia inasema hivi: *"Akafanya yaliyo mema machoni pa Bwana, akaenda katika njia zote za Daudi babaye..."* (**2 Wafalme 22:2**).

8. Timotheo
Timotheo alikuwa kijana aliyefanikiwa sana kiroho na kiongozi aliyeteuliwa kuongoza kanisa katika umri mdogo. Alipata mafanikio katika kazi yake ya huduma kiasi cha kutajwa na mtume Paulo kama msaidizi wake mkuu.

Biblia inasema: *"Mtu asidharau ujana wako; bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi, katika mwenendo, katika upendo, katika imani, katika usafi."* (**1 Timotheo 4:12**).

9. Binti Mariam Mama aliyemzaa Yesu
Huyu dada aliitwa na Mungu akiwa binti kijana(teenager). Kupitia unyenyekevu na utii wake, alifanikiwa kupata hekima na upendeleo wa kipekee.

Biblia inasema: *"Maria akasema, Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema."* (**Luka 1:38**).

10. Msichana wa Kazi wa Naamani
Aliyekuwa mtumishi mdogo katika nyumba ya Naamani. Ingawa alikuwa mtumwa (kijana mdogo), alionyesha hekima iliyofungua njia ya muujiza wa uponyaji kwa bwana wake na kumpa kibali katika jamii.

Biblia inasema: *"Akamwambia bibi yake, Laiti bwana wangu angekuwa pamoja na yule nabii aliye Samaria! Basi angemponya ukoma wake."* (**2 Wafalme 5:3**).

B) Sababu 10 za Kwa nini Vijana wa Kipentekoste ni Maskini wa Kifedha.

Zifuatazo ni sababu 10 kuu zinazochangia vijana walokole kuendelea kuwa maskini wa kipato Tanzania:

1) **Mtazamo hasi kuhusu fedha na utajiri**
   Walokole Vijana wengi wanaamini kuwa kupenda au kutafuta fedha ni dhambi. Wanachanganya mstari wa Biblia unaosema "shina la uovu ni kupenda fedha" na kudhani kwamba kuwa maskini ndiyo kuwa mtakatifu. **1 Timotheo 6:10**.

2) **Kutegemea miujiza ya fedha bila kufanya kazi (Maombi bila vitendo)**

Kuna tabia ya kushinda madhabahuni wakiomba miujiza ya kifedha badala ya kwenda sokoni kufanya kazi. Maombi yanatakiwa yabariki kazi ya mikono yako, lakini kama hakuna kazi, hakuna kitakachobarikiwa **(Yakobo 2:20)**

3) **Ukosefu wa stadi za kifedha na biashara makanisani**

Vijana Wengi waliookoa wanajua sana mambo ya kiroho; lakini hawana elimu ya msingi ya fedha. Makanisani Asilimia 90% ya muda wa ibada zote ni masuala mengine ya kiroho Zaidi. Masuala ya fedha hayafundishwi madhabahuni. Asilimia kubwa kama siyo 95% hawajui jinsi ya kuweka akiba, kuwekeza, kusimamia bajeti, au kukuza mtaji, na hivyo hata wakipata fedha huzipoteza haraka bila kujua zinakopotelea kwenye mifuko iliyotoboka. **Hagai 1:6**.

4) **Matumizi mabaya ya muda kwenye shughuli za kanisa**

Vijana kujitolea kanisani ni jambo jema, lakini kupoteza muda siyo sawa kwa kijana aliyeokoka. Kushinda makanisani kuanzia Jumatatu hadi Jumapili bila mpango unaoeleweka ni hatari sana. Kupoteza muda badala ya kuuokoa, ni hatari kwa maendeleo ya vijana. Kama unataka kufanikiwa, Tumia muda wako kujisomea, kujifunza ujuzi mpya, au kusimamia biashara zako, na kusababisha uzalishaji wao kuwa mdogo sana.

5) **Kusubiri "Sauti ya Mungu" kuanza fursa**

Wakati mwingine uoga unajificha nyuma ya neno "nasubiri kibali au maono." Wanachelewa kuchangamkia fursa za kiuchumi zinazojitokeza mbele zao wengi wakiamini kuwa kila hatua ya kibiashara lazima ije kwa njia ya mafanuo, ndoto au unabii wa moja kwa moja.

6) **Presha ya kutoa fedha kupita uwezo wao**

Kutokana misukumo ya marafiki na wapendwa pamoja na mafundisho makanisani yanayokazia zaidi utoaji ili kubarikiwa, baadhi ya vijana hutoa pesa hata kutoa mitaji yao ya biashara au akiba zao za dharura kama sadaka ya mbegu, kujimaliza, n.k. Hii inawaacha bila akiba ya kuwawezesha kupata maendeleo endelevu. Angalia sana marafiki wanaokuzunguka. Jitahidi uwe BAHILI usitoe pesa ovyo. Vinginevyo utabaki hivyo hivyo mwaka hadi mwaka.

7) **Kupuuza au Kukataa elimu ya fedha na Elimu ya kawaida.**

Makanisa mengi yamejaa watu ambao wana mtazamo wa kudharau elimu ya fedha au ujuzi wa kitaalamu wakiamini kuwa "upako" pekee unatosha kufungua milango yote. Katika ulimwengu wa sasa, soko linahitaji watu wenye weledi, ujuzi wa kiteknolojia, na ubunifu mkubwa.

Ukipuuza au kukataa elimu, maarifa na teknolojia utaachwa na dunia itakukataa HOSEA 4:6.

Elimu ya juu, Maarifa na akili ya juu hutolewa na Mungu mwenyewe kama yanenavyo maandiko yenyewe.

"Naye amemjaza Roho wa Mungu, katika hekima, na uelewa, na maarifa, na ufundi wa kila namna; ili ***abuni kazi za ustadi****, afanye kazi ya dhahabu, na ya fedha, na ya shaba."* (**Kutoka 35:31-32**).

Elimu ya Ubunifu na ugunduzi wa kisasa hutoka kwa Mungu **Mithali 8:12:** *"Mimi, hekima, nimefanya busara kuwa maskani yangu; nami natafuta maarifa ya* ***mambo yaliyobuniwa kwa akili****."*

Ukisoma katika Kitabu cha **2 Mambo ya Nyakati 26:15** utaona kuwa Ubunifu katika Mifumo na Teknolojia. Akiwa kijana, Uzia kama Kiongozi wa nchi, kiongozi kijana kabisa, alitumia ubunifu kuimarisha ulinzi na uchumi wa nchi yake:

"Huko Yerusalemu akafanya mitambo, ***iliyobuniwa na mafundi****, iwekwe juu ya minara... ili kupiga mishale na mawe makubwa."*

Mithali 22:29: *"Je! Wamwona mtu mwenye bidii na ustadi katika kazi zake? Huyo atasimama mbele ya wafalme; hatasimama mbele ya watu wadogo."*

8) **Mtandao finyu wa kijamii (Kujitenga na Watu wenye Fedha)**

Vijana wengi walokole wanajifungia kwenye mzunguko wa watu wa makanisani mwao tu. Wanajiepusha kushirikiana na watu waitwao "kidunia," jambo linalowafanya wakose fursa kubwa za kibiashara, ushauri wa kiuchumi, na masoko mapana yanayopatikana nje ya mfumo wa kanisa. Marafiki wanaokuzunguka kama ni maskini wote,

9) **Kuchumbia Wasichana Wengi (Wapenzi wengi):** Vijana wa kiume wengi huchumbia wasichana wengi na hujikuta wakitumia fedha nyingi kuwasaidia wachumba wao. Vijana wa kiume hutaka kujitutumua ili kujionesha kuwa wana fedha. Wanampa huyu. Wanampatia fedha yule. Mpaka mitaji yao inapukutika.

10) **Kununua makorokoro Mengi:** Mara mkufu. Mara mkoba. Mara umenunua saa. Mara umenunua kiatu. Mara miwani. Mara gari mkweche. Mara bodaboda. Mara kula chipsi. Mara kwenda beach. Mara nguo hii au ile. Maandiko yanatuasa ifuatavyo:

Mhubiri 2:11 Epuka kutumia fedha yako katika vitu visivyokuwa na tija ili usiwe kama Sulemani aliyehitimisha kwa kusema **:** *"Kisha nikaziangalia kazi zote zilizofanywa na mikono yangu, na taabu yote niliyofanya ili niifikie; na tazama, yote yalikuwa ubatili na kufukuza upepo, na hakuna faida yoyote chini ya jua."*

Mithali 13:7: Epuka kujionyesha kuwa una vitu vya maana hata kama utapata fedha nyingi sana ili uende na hekima hii ya Sulemani**:** *"Kuna mtu ajifanyaye kuwa tajiri, kumbe hana kitu kabisa; Kuna mtu ajifanyaye kuwa maskini, naye ana mali nyingi."*

Luka 12:15 (Onyo la Yesu kuhusu kulundika vitu): *"Akawaambia, Angalieni, jilindeni na choyo, maana uzima wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo."*

===================End of Day One=====================

DAY TWO:

SOMO: KUJENGA NGOME ZA UTAJIRI UDUMUO KAMA VIJANA WALIOOKOKA

(Building A Strong Financial System Strongholds)

Recap of Day One:

Maswali kwa Darasa:

1. **Taja sababu zinazowafanya Vijana wengi waliookoka kutokuwa matajiri?**
2. **Umejifunza nini siku ya kwanza ya Semina?**

A) Mbinu Walizotumia Vijana wa Zamani za Biblia Kuwa Matajiri

i) Kuwekeza 20% ya Mapato yote unayopata

Kijana yusufu alilifanya taifa zima la Misri kuwa na chakula kingi sana kama inavyosimuliwa Katika Kitabu cha Mwanzo 41. Tunaona jinsi Mungu alivyomfunulia Yusufu kanuni ya kujiokoa na kuliokoa taifa la Misri, familia ya Yusufu, na Mfalme Farao na mataifa yoye ya wakati huo. Yusufu alitumia mbinu zifuatazo kufanikiwa sana

Kuweka Akiba 20% ya Mavuno wakati wa Utele: Yusufu aliwashauri Wamisri kukusanya sehemu ya tano (asilimia 20) ya mazao yao yote katika miaka ya shibe na kuyahifadhi kwenye miji. Huu ni wajibu wa kiuchumi: kujiandaa kwa siku za usoni ukiwa bado na nguvu na kipato.

Matumizi Sahihi ya Rasilimali: Katika nyakati za shida, akiba hii iliokoa maisha ya Wamisri na mataifa yaliyozunguka. Kijana anapaswa kutambua kwamba nyakati za wingi hazimaanishi matumizi ya anasa, bali ni nyakati za kujenga msingi wa dharura.

ii) Kufanya Kazi na Kuwekeza Kwa Bidii bila Kusubiri Kusukumwa:

Mithali 6:6-8 Vijana wote waliofanikiwa katika Biblia walifanya kazi kwa bidii kama mchwa kwa nidhamu ya fedha na mali kama mchwa au chungu anavyofanya kazi usiku na mchana.

Kujiongoza na Nidhamu: Ukitaka ufanikiwe kifedha kama vijana wa zamani wa Biblia ni lazima ufanye kazi kama Mchwa. Wao hawana kiongozi wala msimamizi anayewalazimisha kufanya kazi, lakini wanafanya kazi kwa bidii na kutunza akiba wakati wote. Kijana aliyekomaa kimaisha hafanyi kazi kwa sababu anasimamiwa, bali anasukumwa na malengo yake.

Kujiandaa kwa Baadaye: Kama unataka kufanikiwa sana hakikisha haufanyi kazi kwa bidii tu, bali fanya kuweka akiba ya chakula kama mchwa wanavyofanya hutunza chakula chao ili ikifika wakati wa

jua na kiangazi kirefu wasikose chakula. Kijana anapaswa kuwekeza na kuweka akiba ya fedha leo ili zitunze maisha yake wakati wa uzee, ugonjwa, au changamoto za uchumi.

iii) Vijana wa Biblia waliweka Akiba Mahali Salama.

Kama unataka kufanikiwa hakikisha unaweka akiba ya fedha itakayokufaa wakati wa hali mbaya kama vile biashara kusimama, wateja kupeperuka, siasa za nchi kubadilika, misiba ya kuhitaji fedha nyingi, n.k. Hili ni jambo ambalo vijana hulipuuzia wakidhani mambo yatabakia kuwa kama yalivyokuwa jana.

Ndiyo maana inapotokea miaka ya njaa vijana wengi huondoka mijini na kurudi vijijini walikotoka eti kwenda kujipanga upya. Lakini hiyo siyo hekima tunayojifunza kwa vijana wa Biblia waliopambana kubadilisha hali ya uchumi wao.

Mimi kama Mwalimu wa fedha, naomba nikushauri na kukupa maarifa ya kuweka akiba kubwa ya fedha enye faida ambazo zitailinda thamani yake dhidi ya mfumuko wa bei:

a) **Akaunti za Benki:** Salama kwa dharura za muda mfupi na zinazoweza kufikiwa kwa urahisi.Mfano benki ya CRDB, NMB, TCB, AZANIA, N.k. Utakuwa na faida ya 3% hadi 7% kwa mwaka kama utafungua akaunti ya akiba maalum.

b) **Mfuko wa Dharura**: Mfuko wa dharura ni Mfuko unaokuwa unaweka akiba zako kila siku au kila wiki au kila mwezi unapopata pesa. Akiba ya dharura ni fedha kwa ajili ya matukio makubwa tu. Matukio hayo ni kama: Ugonjwa unaohitaji Matibabu Makubwa, Biashara kuyumba, Kufukuzwa Kazi, au lolote kubwa ambalo hukulitegemea kutokea.

   Unaweza kufungua akaunti ya fedha ya dharura kwenye Mfuko wa M-WEKEZA na FADEMO Lulu Investment Fund (www.fademo.co.tz) au pakua App ya FADEMO kwenye Playstore/Appstore ambapo unaweza kuwekeza muda wowote kiasi chochote kuanzia TZS 5,000 na ukawa unavuna faida kila mwezi.

   Kijana wekeza pesa unayopata ya ziada kwenye M-WEKEZA au Fademo Lulu Investment Fund ambapo unaongezewa kila mwaka faida ya 12% au 13%.

   Vijana wote tangu wa zamani waliofanikiwa kama akina Yusufu, waliweka akiba ya angalau 20% ya mavuno au fedha au dhahabu na ndiyo maana walifanikiwa. yako.

c) **Weka Akiba Katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii/Pensheni:** Ni Muhimu kwa ajili ya ulinzi wa muda mfupi na muda mrefu wa maisha yajayo. Mfuko wa Fademo Social Fund ni mfano mzuri wa Mifuko ya Jamii na Pensheni kama ilivyo NSSF na PSSSF.

Unaweza kujiunga na Mfuko huu wa Fademo Social Fund (FSF) kwa kutumia mitandao ya simu na Benki kwa kianzio cha Shilingi 10,000 kwa mwezi. Kama ukichangia kila mwezi shs 10,000 utapata Mafao ya kukulinda wewe na familia yako sasa na baadaye uzeeni. Utapata huduma zifuatazo kama mwanachama wa Mfuko wa FSF:

(i) Fedha ya Hongera kwa Kufunga Ndoa takatifu
(ii) Fedha ya Hongera kwa Kupata Mtoto
(iii) Fedha ya Matibabu ukilizwa siku 3
(iv) Fedha ya Pole na Msaada wa Mazishi ukipatwa na msiba
(v) Fedha ya Pole kwa Kupata Ajali ya gari, moto, n.k
(vi) Fedha ya Kwenda Hospitalini Kuchunguza Afya yako
(vii) Fedha ya Kusapoti Ujenzi wa Nyumba yako
(viii) Fedha za Kusapoti Ununuzi wa gari la ndoto yako.
(ix) Pensheni ya Uzeeni
(x) Mafao ya Wategemezi wako inapotokea kifo

d) Kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa FADEMO unaweza kufanya hivyo kupitia MITANDAO ya simu na mtandao wa FADEMO kwenye website: www.fademo.co.tz hapo utafuata maelekezo ya kujiandikisha kama mwanachama wa Mfuko huu na utaanza kuchangia kila mwezi ili upate Mafao hayo.

e) **Wekeza Kwenye Mali Isiyopungua Thamani (Assets that bring money):** Vijana wa Bibilia waliwekeza kwenye assets kama vile; dhahabu, majengo, mashamba ya mazao, madini,

fedha na shaba. Mahali pengine ambapo kijana anaweza kuwekeza fedha yake anayoipata ni kwenye rasilimali ambazo hukua thamani kila mwaka kama vile mashamba ya mazao ya kudumu, majengo ya biashara, Mazao ya muda mfupi kama vile mbogamboga, mahindi, mpunga, ndizi, n.k. **Angalizo:** Epuka kununua mashamba makubwa yasiyokuletea faida. Bora ununue shamba dogo unaloweza kutunza. Anza kulitumia kwa kulima bustani ya mazao mbalimbali ya kudumu kama vile embe, chungwa, parachichi, pilipili hoho, nyanya-chungu, karoti, mbogamboga n.k.

f) **Wekeza Kwenye Mifuko ya Uwekezaji Pamoja (Fademo Social Fund):** Mahali pengine unapoweza kuwekeza fedha yako ya ziada ni kwenye mifuko ya umoja. Hii ni mifuko ya makampuni binafsi na serikali pia. Kwa sasa kuna mifuko Zaidi ya 20 Tanzania ambayo imesajiliwa na serikali na unaweza kuwekeza akiba yako na ukawa unakula faida itokanayo na akiba yako.

g) **Wekeza Kwenye Hati za Serikali na Makampuni:** Hatifungani za Muda mrefu na Mfupi. Hii niNjia nzuri ya kuwekeza na kukuza mtaji kwa ajili ya utajiri wa baadaye.

iv) Kujilinda na Utumwa wa Madeni

Katika Mithali 22:7, Maandiko yanasema kuwa "akopaye ni mtumwa wa akopeshaye."

Vijana wa zamani za Bibilia walifundishwa kuhusu fedha sana. Waliaswa kujiepusha na Madeni. Tangu nyakati zile wana wa Israeli wako jangwani Mungu aliwaonya kuhusu kujiepusha kwenda kukopa pesa ya matumizi ya kawaida kama vile kukopa kwa ajili ya starehe, simu za gharama, au mavazi.

Mungu alijua kuwa madeni ya aina hiyo yangewafilisi sana na kuanza kuishi kama watumwa kwenye nchi yao. Kama unataka kujikomboa kifedha ushauri wangu ni huu:

a) Acha tabia ya kuishi kwa kukopa, badala yake ukizidiwa omba msaada.
b) Lipa madeni unayodaiwa anza na deni kubwa zaidi kwanza mpaka yote yaishe.
c) Epuka kuwa mdhamini wa mikopo ya watu wengine, kwani hilo ni tundu linalofungua milango ya kufilisika na utumwa au kufungwa (Mithali 6:1-5).

B) Mambo 10 ya Kufanya Vijana wa Kipentekoste Wafanikiwe Kifedha na Kiuchumi

1) **Kupanga Bajeti ya Matumizi:** Vijana wengi hawapangi bajeti. Matajiri wote hupanga bajeti. Ajabu ni kwamba maskini hawapangi bajeti wakisingizia kipato kidogo. Wengi hujikuta wanafanya Matumizi ya kila siku bila mpangilio maalum na mwisho huleta ubadhirifu.

2) **Kuwekeza angalau 20% ya Kila Pesa Unayopata:** Kabla ya matumizi yako ya wiki ay mwezi hakikisha kwanza unaondoa 10%-20% ya kuwekeza akiba yako. Utajiri hujengwa kwa kulipa kwanza akiba yako (angalau 10%-20%) kabla ya kuanza matumizi ya lazima.

3) **Tofautisha Matamanio na Mahitaji:** Kununua vitu kwa sababu ya kuonekana na jamii badala ya uhalisia wa kipato chako. Usinunue vitu visivyokuwa kwenye bajeti. Epuka kununua makolokolo. Nunua vitu vyenye tija kwa familia au uchumi wako.

4) **Anzisha Vyanzo Vinne vya Mapato (Four Sources of Income):** Kijana Kutegemea ajira au biashara moja pekee hakutoshi kujenga utajiri wa . Hakikisha una chanzo mama cha mapato. Na hicho chanzo ukitumie kuanzisha Chanzo cha pili, cha tatu, cha nne na kuendelea. Mungu alimwekea Adamu na Eva mito 4 katika bustani ya Eden ili iweze kutiririsha maji katika Bustani na isiweze kukauka. Hii kiuchumi maana yake ni kuwa na vyanzo angalau 4 katika maisha yako ili Bustani yako (Maisha yako) isikaukiwe fedha. **MWANZO 2:10-14**

5) **Kuepuka Utajiri wa Haraka (Kamari/Kashfa):** Kutafuta njia za mkato badala ya uwekezaji thabiti na uvumilivu. Hauwezi kutajirika kwa kucheza upatu, betting, kuchangiana, na kufanya biashara haramu.

6) **Kuepuka Matumizi ya Anasa:** Ukipata pesa yoyote epuka kuitumia pesa ya mkopo kwenye masuala ambayo hayahusiani na mkopo usiozalisha faida. Usiwe kama mwana mpotevu alieamua kutumia fedha kwa anasa hadi akaamua kula vyakula vya nguru baada ya kufulia fedha yote aliyopewa na mzazi wake kama mtaji. Epuka kutapanya fedha yako kwa wanawake au wanaume. Epuka kujivuruga mwenyewe.

7) **Kujiendeleza kwa Elimu Iletayo Fedha zaidi:** Kutowekeza kwenye akili yako, ni kuamua kufa maskini. Kutosoma kitabu chochote kinachohusu fedha mwaka mzima, ni kujizamisha kwenye tope la umaskini. Kutofundisha elimu ya fedha makanisani, ni kuamua kuwaacha waumini wako waendelee kuwa maskini kifedha ingawa wananena kwa lugha sana na kuimba sana kwaya. Elimu ndiyo mtaji mkubwa wa Utajiri. Maarifa ya kifedha Hupatikana kwa kusoma, kusikiliza, kuhudhuria semina za fedha, n.k. Elimu ya ufundi, umeme, magari, majengo, kilimo, ufugaji, teknolojia, n.k haitakuja kwako kwa kusali sana na kuimba sana. Bali kwa kuamua kufuatilia elimu hiyo.

8) **Kutokuwa na Malengo ya Muda Mrefu:** Kuishi leo bila maono kunawafanya vijana wasijue wanakotaka kwenda kiuchumi. Hakikisha ukiamshwa usiku saa 8 unawea kuwaeleza watu maono yako ni yapi miaka 5 au 10 ijayo. Unataka uwe kama nani? Unataka uwe na kipato gani miaka 5 ijayo. Unataka kuishi maisha ya aina gani? Panga malengo yako mpaka wajukuu wako unavyotaka waje kuishi.

9) **Kuzungukwa na Watu Wasio sahihi (Marafiki/Washauri):** Kuwa na marafiki wanaokushinikiza kutumia fedha kwenye starehe badala ya maendeleo itakudidimiza kifedha. Unashauriwa kuwa makini na marafiki wasiofaa kifedha hata kama wameokoka. Epuka kuchagua mke au mume ambaye hatakuwa na maono ya maendeleo kwenye idara ya fedha. Mke au mume anayewaza kutumia tu na hawazi lolote kwenye Uwekezaji na wala kwenye stori zote husikii akizungumzia uwekeza na maendeleo. Ni dalili tosha kuwa hafai.

10) **Kutothamini Fedha Ndogo:** Kudharau kiasi kidogo cha fedha na kushindwa kufanya uwekezaji Zaidi ili fedha izalishwe na kukuza mtaji na utajiri haitakusaidia kijana wa Kitanzania. Hakikisha hata kama unapata fedha 250,000 tu kwa mwezi uifanyie mpango wa bajeti kwa kuzingatia kanuni ya kutenga pesa ikufanyie kazi. **Matajiri huwaza jinsi gani fedha imfanyie kazi. Maskini huwaza kufanya kazi maisha yote. Ni huzuni.**

C) JINSI YA KUPANGA BAJETI YA KUELEKEA KWENYE UTAJIRI UDUMUO

Tunamalizia semina yetu Kwa kujifunza jinsi ya Kupata bajeti yenye matokeo kwa kutumia mifano miwili au mitatu tu ili kujenga uelewa wa kufanya bajeti zetu za kila siku kama wakristo waliookoka.

Maandiko yanasema kwamba Huwezi kujenga ghorofa bila kupiga hesabu ya gharama za ujenzi wa ghorofa. Utaishia njiani.Wakristo wengi hukwama kwenye masuala mengi kwa kuwa hatupendi kufanya hesabu.

Yesu anafundisha kuhusu kupiga hesabu kabla ya kujenga mnara katika **Luka 14:28-30**, akisisitiza umuhimu wa kufikiria gharama ya jambo kabla ya kulianza ili kuepuka kushindwa na dhihaka.

Mfano huu wa Yesu Kristo, unatufundisha kuishi kwa Bajeti. Anatufundisha kuwa na bajeti kwa kila Mradi tunaotaka kufanya. Maisha ni Project. Usipopiga hesabu ya mapato na Matumizi hautafanikiwa katika biashara zako. Hautafanikiwa hata ukiajiriwa. Piga bajeti kwa kila kitu. Ukiwa na hesabu na bajeti ya chochote unachotaka utakipata.

Mifano Miwili:

BAJETI YA KIJANA ANAYETAKA KUJENGA NGOME YA KUDUMU YA UTAJIRI

Mpangilio wa Bajeti ya Kijana Aliyeokoka

- **50% ya Mshahara = Matumizi ya Lazima ya Familia(Chakula, ada, Kodi, nk.**
- **20% ya Mshahara = Uwekezaji na Akiba ya Baadaye (FADEMO SF)**
- **10% ya Mshahara au Kipato chako = Zaka.**
- **15% ya Kipato chako = Toa Sadaka, Michango ya harusi, Misaada kwa Ndugu.**
- **5% ya Mshahara = Burudani zako binafsi (Soda, nguo, vipodozi,..)**

Mfano Wa Mtu mwenye Kipato cha TZS 350,000

Kama unapata Kwa Mwezi TZS 350,000 Bajeti yako inatakiwa iwe:

1.

TZS	ASILIMA	KIASI	MAELEZO
350,000.00	50%	**175,000.00**	Chakula, umeme, gesi, Ada za Watoto,
350,000.00	9%	**30,000.00**	Nauli za Kwenda Kazini/Kurudi
350,000.00	18%	**60,000.00**	Kodi ya Nyumba
350,000.00	10%	**35,000.00**	Akiba na Uwekezaji FADEMO
350,000.00	10%	**35,000.00**	Zaka ya Mungu
350,000.00	4%	**10,500.00**	Sadaka, Michango, harusi, kujipa raha, n.k

BAJETI YA MSHAHARA WA TZS 500,000/=

BAJETI YA MATUMIZI MSHAHARA WA 500,000/=

1) KODI YA NYUMBA = 120,000 (Chumba kizuri maeneo salama)
2) UMEME = 20,000
3) MAJI = 10,000
4) MKAA/GAS = 30,000
5) CHAKULA (GETO) = 160,000
6) USAFIRI = 50,000
7) VOCHA = 20,000 (Inatosha kwa data na kupiga simu)
8) AKIBA = 60,000 (Usiache kuweka akiba FADEMO kila mwezi)
9) ZAKA/SADAKA = 15,000
10) MATUMIZI BINAFSI = 15,000

JUMLA: 500,000/=

Ushauri: Nusu milioni ni hatua nzuri! Linda akiba yako na anza kufikiria jinsi ya kuwekeza hiyo akiba kwenye hisa (FADEMO LULU FUND). Tengeneza chanzo cha *kipato cha ziada kwa kila mwezi upate pesa ya tofauti na Mshahara au biashara.*

Unawezaje kutengeneza utajiri kupitia FADEMO LULU FUND?

Ukiamua kuwekeza Tsh 100,000 kila mwezi kupitia FADEMO LULU kwa muda mrefu, matokeo yanaweza kuwa hivi:

- **Miaka 10 👉 23.5M**
- **Miaka 15 👉 50M**
- **Miaka 20 👉 96.5M**
- **Miaka 25 👉 178.5M**
- **Miaka 30 👉 325M**

🧠 **Tajiri si lazima aanze na mamilioni. Anza na kidogo, endelea bila kukoma.**

Mfano wa Shamba la ekari mbili unavyoweza kuligawanya ukalima kwa faida kubwa. Unaweza kugeuza shamba lako kuwa kama BUSTANI YA EDENI.

MAWASILIANO

MR. JUMA MILINGA: 0767 285 417 (Calls)

0768 201 749 (WhatsApp)

Social Platforms: Facebook: Venerando Milinga

YouTube: Fademo Online TV

WhatsApp Group: WASTAAFU WOTE FORUM

MWISHO